AL BAYAAN DAAWAH MEDIA

منهج السلف الصالح

# DAAWAH NA MITANDAO YA KIJAMII

Dawah, kwa ufahamu wa kiislamu ni njia ya kulingania na kuwaalika au kuwaita watu kuelekea katika wito wa kiislamu kwa kumuabudu Allah subhaanahu wataala peke yake na kufuata maamrisho yake.

## MITANDAO YA KIJAMII.

Imesaidia sana kuwezekana kusambaza ujumbe wa kiislamu na sasa imekuwa wajibu wetu waislamu kutumia uwanja huu vizuri kufanya daawah .Kwa hakika kwa sasa ndio moja ya uwanja bora kufanyia daawah katika zama hizi za utandawazi.

# UWANJA WA MITANDAO YA KIJAMII.

Uwanja maarufu kwa watu wengi kufanyia Daawah kupitia mitandao ya kijamii ni kama facebook,twitter ambayo sasa hivi inaitwa X,Youtube,whatsapp,na mengine.

Mitandao yote hii ingawaje zinatafautiana kimfumo lakini hutumika kama uwanja wa watu kukutana. Imefanya dunia kuwa kama kitu kimoja. Leo hii unaweza pata khabari yanayojiri mataifa mengine kupitia mitandao ya kijamii.

Mitandao hii inawezekana kua khasa  za watu kujumuika pamoja kama vile Facebook,whatsapp na linkedln; maeneo ya mjumuiko kama twitter', mijumuiko ya kuchangia picha Kama snapchat,printerest na instagram.'kuchangia picha kama youtube au kuchangia elimu kama Quora.Mlinganiaji mwenyewe kulingana na uhitaji wake anaweza kutumia mfumo utakaomnasibu kulingana na mahitaji yake .

Ujumbe wa Daawah unaweza kufikishwa kwenye facebook kwa njia nyingi kama vile ujumbe wa kimaandishi,video na kwa sauti (audio). Facebook live kwa maana ya mubashara Pia ni mojawapo wa njia ya kuwasiliana na watu wengi moja kwa moja na ni njia nyepesi na yenye gharama ndogo. Facebook pages kwa maana ya ukurasa wa facebook na magrupu mengine ya mitandao ya kijamii ni mojawapo wa mifumo au uwanja mzuri wa kufanyia Daawah.

Twitter ambayo sasa hivi inajulikana kama X Ni mojawapo wa mifumo mizuri ya mawasiliano ya kijamii ambayo ni maarufu na kubwa ambayo inaweza kuwa ya pili baada ya facebook. Ni mojawapo wa njia kubwa sana inayoweza kutumika kufanya Daawah na kuwafikia watu wengi zaidi kwa wakati mmoja.

YouTube Ni mojawapo wa uwanja mkubwa na bora kuweza kufikisha ujumbe wa Daawah kupitia njia ya video. Watu wengi wanapenda waone matukio kwa njia ya video Ni vyema pia kutumia uwanja huu kusambaza ujumbe wa kiislamu. Watu wengi

wamefungua channel zao za Daawah kupitia Telegram,youtube ambayo wamefungua ON LINE TV..facebook page ya Daawah n.k.

## BAADHI YA FAIDA NI KAMA:

1. Uwezo wa kuwafikia watu wengi kwa wakati mmoja.

Waislamu wengi wanatumia mitandao ya kijamii vizuri kwa kufikisha ujumbe wa kiislamu . Watu wanapata faida kwa kubonyeza tu link husika. Watu wengi wanafikiwa na kuletwa pamoja kupitia mitandao ya kijamii. Ni njia pia ya kuwafikia wasiokua waislamu.wanazuoni wengi hutumia fursa hii kuweza kujibu au kutatua maswali yenye utata khasa kwa wasiokua waislamu. Mifano mizuri ya kuigwa hapa kwetu ya kueneza dini kupitia mitandao ya kijamii ni kama kishki TV na wengine wengi waliofungua ON LINE TV na Channel mbalimbali.

2. Ni njia nyepesi ya kufikisha Daawah. Masahaba walikua wakipanda juu ya farasi kama njia ya kufikisha Daawah kwa mikusanyiko ya watu. Leo tunaweza kuwafikishia watu wengi ujumbe wa Daawah kwa watu wengi na kwa wakati mmoja kwa wepesi. Ukitaka unaweza kufikisha ujumbe kwa mfumo wa kimaandishi,video au audio.

3. Hajj na Ramadhan
Hizi ni nyakati ambazo watu wengi ulimwenguni hutumia mitandao ya kijamii kufikisha elimu kuhusu Hajj na saumu ya ramadhani. Siku hizo utaona watu wengi facebook,twitter,whatsapp,instagram na mitandao yao mengine ya kijamii imesheheni Daawah kuhusu uislamu. Taratibu hizi zimeongezea uwepo wa Daawah kwa njia ya kisasa na kwa kizazi kipya cha kisasa. Wakati wa Ramadhan utaona watu wengi wanasambaza elimu kuhusu fadhila za ramadhani kama vile kufuturisha na mengine. Wakat wa hajj utaona wengine wanasambaza ujumbe kuhusu kuhiji. Yote

haya ni matumizi mazuri ya mitandao ya kijamii kusambaza ujumbe wa kiislamu.

4. Inalinda uislamu kudhaniwa vibaya.

Mitandao ya kijamii tunaelezea ukweli kuhusu uislamu na hata wasiokua waislamu wenye fikra potofu kuhusu uislamu,wanaelewa vizuri kuhusu uislamu. Inasaidia kurekebisha fikra au ufahamu potofu ya makafiri dhidi ya uislamu.
Kila mtu ana nafasi ya kugeuza mtandao wake kuelimisha jamii yake kuhusu uislamu.jamii yake yaweza kuwa ndugu zake, familia yake,ukoo wake au kabila lake au watu wote kwa ujumla. Kile kidogo ulicho nacho mfikishie mwenzako. Amesema mtume wetu Muhammad rehma na amani zimshukie kuwa “ Mbora wenu ni yule ataekae soma Qurani kisha akawafunza wengine “ na pia amesema mtume wetu Muhammad rehma na amani zimshukie kuwa “ Nifikishieni kwa wengine kutoka kwangu hata kama ni aya moja”

Mitandao ya kijamii Ni njia nyepesi na nzuri kwa matumizi ya Daawah.Kwa hivyo tutumie fursa hii vizuri wala sio vibaya. Mitandao ya kijamii inaweza kua halali kwako ukitumia vizuri na pia inaweza kua haramu kwako ukitumia vibaya.

5. Mitandao inaongeza wigo wa kupata elimu au maarfa zaidi.

Elimu ya dini imekua rahisi Kupata kupitia mitandao ya kijamii. Leo tunapata maarifa na elimu ya kidini kupitia telegram,youtube na kadhalika. Inawezekana kuna baadhi ya wanavyuoni hujawahi kukutana nao lakini elimu yao unapata kupitia mitandao ya kijamii. Pia kumbukumbu ya elimu yao huhifadhiwa vizuri kupitia mitandao hii.

## BAADHI YA HATARI AU HASARA YA MITANDAO YA KIJAMII:

1. Elimu nusu isiokamilika.

Baadhi ya watu wanajiita wanazuoni lakini elimu zao hazijakamilika na hii inapelekea wafikishe ujumbe wa kiislamu ndivyo sivyo. Wanakua wapotoshaji badala ya waelimishaji. Baadhi ya mashekhe wa mitandao wanaweza kuwa sumu au tatizo kwa jamii kwa sababu ya elimu yao ambayo haijakamilika . Inawezekana wakawa na nia njema ya Daawah lakini wakawa na ufahamu usio sahihi.

## 2. FURSA INAYOTUMIKA VIBAYA.

Watu wengine wanatumia vibaya uwanja huu ili kuvutia watu (Likes au followers ) badala ya kufanya Daawah ya kiuhalisia yenye ikhlasi. Kwa mfano wengine huonyesha picha yenye ushuhuda wa uongo kuonyesha maajabu au karama. Wengine huonyesha picha kuhusu mambo yao ya faragha ambayo hayastahiki watu wengine kuona.

## 3. KUHAMA KUTOKA KWENYE UHALISIA NA KUELEKEA KWENYE MAMBO YA KISASA .

Kuna mambo mengi sana watu wanaiga ambayo ni ya kimagharibi na wala si ya kiislamu kwa kumuiga mtume wetu muhammad rehma na amani zimfikie. Mitandao hii imewafanya wengi kubadilika na kuiga umagharibi badala ya uislamu.

## 4.FILAMU ZA NGONO (Pornography)

Hata kama una ukurasa wa Daawah ni ngumu sana kuperuzi bila kuona au kukutana na picha za ngono. Vitu hivi ni ngumu kuepuka. Kuna mitandao ambayo watu wameweka ili kumkufuru Allah subhaanahu wataala. Wengi wanalazimika kuona mambo ambayo hayafai kabla ya kufikia makusudio ya Daawah. Macho yanapotazama mambo ya haramu,hua inaathiri au kuua moyo ili isiwe salama. Hufanya imani ya mtu ishuke.Mambo haya humfanya mtu kua karibu na shetani na kua mbali na Allah subhaanahu wataala.

## 5. INAONGEZA KUWEPO KWA HADITHI NYINGI ZA UONGO.

Mitandao ya kijamii imekua uwanja wa kueneza uvumi wa uongo na kusambaza khabari zisizo kuwa sahihi. Makafiri wanatumia pia njia hii kuleta khabari zao zisizo kuwa za kweli.

## 6. MAUDHUI YASIOKUA SAHIHI.

Watu wanatakiwa kuwa na uhakika wa yale wanayoweka mitandaoni. Ni lazima kufuatilia usahihi wa hadithi au maudhui husika.Wengi hawazingatii usahihi wa maudhui yao.
Baadhi ya watu wanatoa nukuu zao kwenye hizi mitandao na kujipata wamepata elimu isiokua sahihi.
Mashekhe au viongozi wa mitandao hii wanakua wanapotosha watu kwa sababu wao tayari washapotoka. Elimu yao inakua haija hakikiwa vizuri na mashekhe wanaokubalika kuwa wana elimu.

## 7. UPOTOSHAJI KUHUSU UISLAMU?

Mitandao ya kijamii imetengeza uwanja wa watu kueneza uvumi na uongo au upotosshaji kuwa uislamu ni dini ya ugaidi. Pia kumekuwepo upotoshaji kuhusu waislamu wenye siasa kali .

Uislamu ni dini ambayo inakaribisha maendeleo yote ya kisayansi ambayo hayaendi kinyume na sheria ya kiislamu
Ni wajibu wetu kama waislamu kuangalia mifumo hii kama haiendi kinyume na uislamu
Hatungeweza kuwajua maulamaa wengine ulimwenguni na elimu zao isipokua kwa uwepesi wa hii mitandao. Kwa hivyo tutumie uwanja huu vizuri.
Tunatakiwa kutumia vizuri kwa kuhakiki maudhui kwa kunukuu kutoka kwa wema waliotangulia. Tutumie mitandao hii vizuri na itakua na manufaa.

Kila unapofungua simu yako utaona kua kuna fursa ya kufanya Daawah.  wengine kama baadhi ya kina dada hutumia vibaya fursa hii kama kurusha picha zao

mitandaoni,au mtu kujifanya kuiga msomaji fulani wa qurani au kuimba wimbo wa mwanamziki fulani,au kujifanya msanii fulani. Watu wengine hurusha mambo yasiokua sahihi au ku changia maudhui yasiokua sahihi.wengine kazi yao ni ku share au ku forward maudhui hata yasiokua sahihi. Kwenye ma grupu ya mitandao ya kijamii kuna watu hawana mchango wowote wa kuhakiki zaidi ya kushare au ku forward kwenye ma grupu mengine yale yasiokua sahihi ambayo wamenukuu kutoka kwenye magrupu mengine.

Mitandao inafaa iwe sehemu ya kupeana nasaha ili tujirekebishe tulipokosea. Kwa hakika tunaona katika zama hizi za mitandao nasaha kutolewa na wakati mwingine sio kwa nia ya kurekebisha bali kwa nia ya kukejeli au kutaka sifa (Kiki).

USHAURI NA MAONO(VISION) YETU.

Kuanzia sasa hivi killa mmoja wetu atumie ukurasa wa mitandao yake kufanya daawah au kutoa nasaha za kidini kwa watu au grupu zake.Kile kidogo ulichonacho unachokijua kwa uhakika wake,wafikishie watu wako.sio lazima uwe Mwanachuoni mkubwa.Tusaidiane kusafisha na kurekebisha mitandao yetu ya kijamii. Tusipofanya hivyo,basi watu waovu wataendelea kutawala hii mitandao. Kazi hii ifanywe na watu binafsi na pia makundi au taasisi mbalimbali. Mambo haya yatakufaa kwa sasa na hata baada ya kufa. Tusiwache nyuma kumbukumbu mbaya bali tuwache nzuri.

Mashekhe na maustadhi pia watumie fursa ya mitandao hii kufikisha daawah. Ni sehemu nzuri ya kuweza kuhifadhia kumbu kumbu za elimu yetu.Leo utapata kuna vitabu vingi vya dini katika mfumo wa e book,on line islamic course na elimu ya dini katika mifumo mbalimbali ya mitandao ya kijamii kwa lugha mbalimbali. Kuna baadhi ya maustadh

wanafundisha watu kupitia on line channels mbalimbali.

Ipatikane watu watoe elimu kwa maustadh namna ya kutumia hii mitandao. Tunaona wengine wanatoa khutba ya ijumaa live kupitia ukurasa wao. Utaona kwenye facebook matangazo mbalimbali ya mihadhara ya dini au ujio wa shekhe fulani eneo fulani.Haya ni matumizi mazuri ya mitandao ambayo taratibu yanachukua nafasi ya redio na televisheni.